TANGAZO LA SERIKALI NA. 447 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA UFUGAJI NYUKI
(SURA YA 224)

---

**AMRI**

---

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 11(1))*

AMRI YA KUTANGAZA HIFADHI YA NYUKI YA TAIFA MIALO - KWAMTORO YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Hifadhi ya Nyuki ya Taifa Mialo - Kwamtoro ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Hifadhi ya Nyuki ya Taifa Mialo - Kwamtoro.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA KONDOA


HIFADHI YA NYUKI YA TAIFA MIALO - KWAMTORO

*Makadirio ya eneo*: Hekta 608 au Kilometa za Mraba 6.08

Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la ardhi ya mataji wazi awali chini ya Msitu wa Mialo - Kwamtoro linalopatikana wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2937 ya mwaka 2019 (Skeli 1:20,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 447 (Linaendelea)*




Dodoma,
__24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI
*Waziri wa Maliasili na Utalii*